



**WANAWAKE
WANATAKA
NINI !**

*Wanahitaji Huduma Bora Huduma
za Afya ya Uzazi kutoka kwa
Wanwake na Wasichana*

Madawa na Vifaa. Heshima Afya bora zaidi, ustawi huduma za afya ya uzazii na hata za afya ya kawaida. Vituo vya Afya viongezwe na vifanye kazi kwa ukamilifu, na viwe karibu na wananchi walio wengi. Ushauri Nasaha na elimu kuhusu Afya ya Uzazi na huduma nyingine za Afya vitolewe kwa wananchi. Taarifa wakati wa Uchungu na Kujifungua kuhusu Wafanya kazi wa Afya, Huduma na Vifaa. Wafanya kazi wenye stadi waongezwe na wapatiwe mazingira mazuri kuwezesha kazi zao. Wakunga na Wauguzi wenye stadi zaidi waongezwe na wawezeshwe kufanya kazi zao Maji safi, Maji taka, Vyoo na Usafi. Vitanda na Matandiko ni Muhimu Vifanye Kazi.

**SIKLIZA NA CHUKUA HATUA
KUWAPA WANAWAKE NA
WASICHANA MAHITAJI YAO**



Wanawake Wanataka Nini

Madai ya Huduma Bora za Afya Kutoka wa Wanawake na Wasichana wa Tanzania

Takribani wanawake na wasichana 300,000 duniani wanafariki kutokana na matatizo ya uzazi kila mwaka. Hapa Tanzania vifo vitokanavyo na matatizo ya uzazi vinachangi asilimia 18% ya vifo vyote vya wanawake wenye umri kati ya maika 15-49. Kubadilisha mwonekano huu lazima tuanzie kwa wanawake na wasichana wenyewe. Wanawake wakihusishwa katika kugundua vizingiti na suluhisho za huduma za afya, maendeleo hutokea kwa haraka. Kwa vile ubora wa huduma za afya unachangia kwa kiasi kikubwa kwamba mwanamke atatafuta hizo huduma au la, moyo wa kampeni ya Wanawake Wanataka Nini (*What Women Want*), unalenga kuelewa ubora wa huduma kwa mtazamo wa wanawake na wasichana wenyewe.

Tarehe 11.4. 2018, Siku ya Kimataifa ya Afya ya Uzazi na Haki na kuendelea kwa mwaka mmoja, washirika 359 waliwauliza karibia wanawake na, wasichana balehe karibia milioni 1.2 katika nchi 114 kwamba ni nini kipaumbele chako cha kwanza unachoomba kuona/kufanyiwa wakati wa huduma za afya ya uzazi? Kwa kuongozwa na Muungano wa Utepe Mweupe wa Uzazi Salama (White Ribbon Alliance Tanzania), Zaidi ya mahitaji 110,000 yalikusanywa hapa Tanzania tu. Iliwezekna kutokana na nguvu iliyowekwa na washirika wa afya ya uzazi na waliojitolea ambao hawakuchoka kuuliza na kuhakikisha sauti za hawa wanawake na wasichana zinasikika ndani ya jamii na mashuleni.

Kampeni ya Nini Wanawake Wanataka (*What Women Want* campaign) ni ya kipekee sana kwa vile imewauliza wanawake na wasichana wa Tanzania kusema wanachokitaka kifanyike kinyume na kama tungewauliza ni kitu muhimu au kuwapa majibu ya kuchagua. Kwa mfano mama mmoja wa Yombo Vituka alijieleza jinsi alivyokwenda kutafuta huduma katika kituo cha afya cha serikali akiamini ndiko kuna usalama kuliko angelijifungulia nyumabni. Cha kusikitisha ni kwamba wakati anajifungua wauguzi walimfokea na alivyohitaji msaada walimdharau. Matokeo yake, mtoto wake alizaliwa na ulemavu Ombi lake la huduma zenye ubora, utu na heshima lilijirudia rudia kwa maelfu ya wanawake wengine. “Kama wafanya kazi wa afya wangetoa huduma zenye ubora, heshima na utu; hakuna mwanamke hata mmoja angejifungila nyumban” Sauti na mahitaji ya hawa wanawake vinapotea, hawasikilizwi, lakini ni muhimu kutoa huduma za afya ambazo ndizo wanawaka na wasichana wanapenda wapatiwe.

Wanawake na Wasichana wamepaza sauti zao wanataka huduma za afya zenye ubora zaidi. Mhutasari huu unatupatia vipaumbele kumi (10) vya mahitaji kutoka wale walioshiriki kampeni ya Wanawake Wanataka Nini (*What Women Want* Campaign) hapa Tanzania. Kama tegemeo na matazamo wetu ni wanawake na wasichana kweda vituo vya afya, basi inabidi tuzingatie mapendekezo na ushauri wao na kwa pamoja tutafute matokeo mazuri zaidi ya afya. Ieleweke kuwa mategemeo yao lazima yawe mategemeo ya kila mmoja wetu.

Wanawake na Wasichana

Wamekwisha sema,

Sasa ni wakati wa kuwasikiliza.



MIKOA 10

Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Tabora

WASHIRIKA 210

MAHITAJI 111,901

Wasiojulikana (<1%)



Kujifunza zaidi kuhusu utaratibu uliotumika kukusanya takwimu na jinsi tulivyopata majibu, ingia: whiteribbonalliance.org/whatwomenwant ili upate muhtasari wa repoti nzima.

VIPAUMBELE KUMI VYA MAHITAJI

1. Madawa na Vifaa: **8.99%**
 - Upatikanaji wa damu salama na iwe bure*
 - Vifaa vinavyohitajika kwa afya ya uzazi viongezwe
2. Huduma bora zenye heshima na utu: **8.61%**
 - Wafanya kazi wa afya rafiki na wanaojali
3. Huduma za afya ya uzazi na nyinginezo kuwa nzuri ili tuwe na afya bora na ustawi: **7.56%**
4. Vituo vya Afya vinavyofanya kazi kwa ukamilifu na viwe karibu na wananchi walio wengi: **7.32%**
5. Ushauri Nasaha na Elimu juu ya Afya ya uzazi na afya kwa jumla: **7.17%**
6. Taarifa zitolewe kuhusu uchungu na kujifungua, juu ya wafanya kazi, huduma na vifaa: **7.03%**
 - Uwepo wa vifaa vya kujifungulia
7. Wafanya kazi wa afya wenye stadi waongezwe na wawekewe mazingira mazuri ya kufanya kazi: **5.41%**
8. Wakunga na Wauguzi na wenye stadi waongezwe na wawekewe mazingira mazuri ya kufanya kazi: **4.61%**
9. Maji Masafi, Maji Machafu Vyoo na Usafi: **4.41%**
 - Vituo vya Afya viwe na vyoo vya kisasa vya kutosha na viwe safi
 - Maji Safi ya bomba yawepo kila wakati
10. Vitanda na Matandiko: **4.18%**
 - Vituo vya Afya viwe na vyoo vya kisasa vya kutosha na viwe safi
 - Maji Safi ya bomba yawepo kila wakati

* Inawakilisha mafungu ya vipaumbele 10 vya mahitaji

SIKILIZA CHUKUA HATUA

Kuwasikiliza wanawake ni hatua kubwa.


Lakini kufanyia kazi yale tunayoyasikia ni mabadiliko.



Tuambie jinsi unavyowasikiliza na kufanyia kazi mahitaji ya wanawake na wasichana:

whiteribbonalliance.org/whatwomenwant

Picha zote ni mali ya Wanawake Wanataka Nini: Mahitaji ya Huduma za Afya ya Uzazi zeny Ubora kutoka kwa wanawake na Wasichana.



**WHAT
WOMEN!
WANT!**

WANAHITAJI HUDUMA BORA HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI
WANAWAKE
WANATAKA
NINI
KUTOKA KWA WANAWAKE NA WASICHANA